

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA NNE

25 APRILI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA NNE – TAREHE 25 APRILI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

178. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni haja ya mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri kutolewa kwa Mjasiriamali mmoja mmoja.

179. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Kituo cha Afya cha Nhobola kitafanyiwa ukarabati ikiwa ni pamoja na upanuzi baada ya kuwa chakavu kwa kipindi kirefu.

180. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, vikwazo gani vinasababisha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kyela usipandishwe hadhi kuwa Halmashauri ya Mji.

181. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka mashine ya X-Ray katika Hospitali ya Manispaa ya Mpanda.

WIZARA YA NISHATI:

182. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itakamilisha kusambaza umeme wa REA kwenye Vijiji 20 vilivyobaki - Mkalama.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

183. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini ujenzi wa Chuo cha Uvuvi na Mifugo utaanza katika Kata ya Igamba – Mbozi.

184. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha na Wataalam katika eneo la Mbongo Kata ya Manda ambalo linafaa kwa ufugaji wa Samaki kwenye Vizimba.

WIZARA YA KILIMO:

185. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itarejesha Kiwanda cha Chai cha Wakulima wa Lupembe Muvyulu.

186. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani wa kukarabati Mabwawa ya Naipingo, Chemchem, Mkumba, *Farm Four* na *Eight*, Ntila na JKT Nachingwea.

WIZARA YA FEDHA:

187. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kwa nini Kodi ya Jengo na Kodi ya Ardhi zisiunganishwe na kuwa moja ili kumuondolea usumbufu Mwananchi.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
25 APRILI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**